

# Mpendwa wako aliyefariki anaweza kusaidia kupata suluhu za COVID.

Pole sana kwa kifo cha mpendwa wako.

Kwa kujiunga na utafiti wa uchunguzi wa maiti, mpendwa wako anaweza kutusaidia kujifunza kuhusu athari za kudumu za COVID kwenye afya kwa njia ambazo haziwezekani ikiwa angekuwa hai.

Uchunguzi wa maiti ni uchunguzi wa kimatibabu unaofanyiwa mwili baada ya kufariki. Haitachelewesha mazishi wala kuathiri shughuli ya kutazama mwili. Wakati wa uchunguzi wa maiti, madaktari wanamshughulikia mpendwa wako kwa heshima.

## Kwa nini niruhusu mpendwa wangu aliyefariki kushiriki katika utafiti huu?

- Uchunguzi wa maiti unaweza kutusaidia kuelewa kilichosababisha kifo cha mpendwa wako na kujua matatizo ya afya aliyokuwa nayo, haya yanaweza kusaidia katika kuomboleza
- Mpe mpendwa wako heshima yake na upate kuridhia kwa kujua wanasaidia watafiti kujua jinsi ya kuzuia na kutibu COVID, haya yanaweza kusaidia kuokoa maisha ya wengine katika siku zijazo



Ili kupata maelezo zaidi, tembelea [RECOVERcovid.org](https://RECOVERcovid.org)



**RECOVER**  
Researching COVID to Enhance Recovery

An Initiative Funded by the National Institutes of Health